Hon. (Ms.) Sidi: Thank you Mr. Speaker. Our second visit was in Malindi Ward where we visited the Central ECD project that was budgeted in the financial year 2015/16. When we arrived at the site we realized that the building had roof leakages and it was of low quality.

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mwarandu what is your Point of Order?

Hon. Mwarandu: Thank you very much Mr. Speaker. I am standing on a Point of Order 102. You see you are forcing us to breach these Standing Orders because what the hon. Member for Mtepeni has said is very correct. The hon. Member is repeating what the Chairperson has said as well as what the Vice Chairperson has said and it is here in the Standing Orders 102. *“The Speaker or the Chairperson of Committees, after having called attention to the conduct of a Member who persists in irrelevance or tedious repetition either of the Member’s own arguments or the arguments”* Mr. Speaker, it has already been said. I think the hon. Member has to follow another route. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Kindly you are out of Order; hon. Humphrey Mwarandu you are out of Order. Kindly take your seat; you are out of Order because the Member has not been irrelevant in her contributions. There is nothing irrelevant; in fact she gave out two issues which had not even been mentioned by the Chairperson or the other...

Hon. Mwarandu: It is irrelevant or repetition. I did not say it is irrelevant; it is repetition...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): You are out of Order. The Standing Order that you gave is talking about repetition but on issues that are irrelevant. She is very much in Order; kindly give her time to make her contributions. She is a strong and able Member of the Education Committee. They did site visits and the information she is giving is very important. Proceed and wind up.

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you Mr. Speaker. Just to proceed, in total we did a sample of 12 ECDs plus polytechnics in all the seven Sub- Counties. If you go through our findings you will find that most of these projects from the financial year 2014/15 in an average of one to ten I would say three percent had been completed but 70 percent is yet to be completed. You will realize that these ECD projects are from the ward development funds kitty. This is a big problem for the members of those wards and also for the children and also on the issue of care givers who are not employed by the County Government. The schools are in pathetic conditions and if you go through our findings you will realize all these issues have been highlighted and we have given a proper way forward. I urge my fellow hon. Members to adopt this Report so that these recommendations can be implemented. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Hon. Ronald Kazungu Mbura kindly make your contributions.

Hon. Mbura: Asante mheshimiwa Spika kwa nafasi hii. Nataka kuunga mkono Ripoti iliyo mbele yetu. Pia kuweza kuunga mkono madai na kuyaweka wazi ya mheshimiwa Peter (Ziro) kwamba ofisi ya *procurement* ya Elimu imezembea sana. Huo ni ukweli na ametaja Ilham

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kwa sababu ni Ilham mwenye kufanya haya lakini ni kwa vile anaongoza ile afisi. Thibitisho ni kwamba mimi kama mheshimiwa wa Chasimba nimeshangazwa muda huu kwa kutafuta wanakandarasi kwamba mradi wa ECD wa Mafisini ulikuwa umepewa wanakandarasi wawili wanaenda sambamba. *Quotations* mbili zinaenda sambamba zikiwa zimefika kwa Matano na nilipouliza Ilham akaniambia ni makosa yamefanyika. Walienda kuketi kwa warsha wakitumia pesa za umma kutengeneza Ripoti na Ripoti ile wakatuletea wanakandarasi wawili wote wakiwa wanapambana na ECD ya Mafisini. *Chief Officer* nilipomuuliza hakunipa majibu yoyote lakini nikaona ya kwamba hali hii si Ilham peke yake bali ni ofisi mzima pamoja na *Chief* wetu.

Kuna tabia ya kwamba unakula kitu kidogo kwa mwanakandarasi na mwengine anakula kitu kidogo kwa mwanakandarasi; sasa mle ndani wanashindana. Biashara za ofisi haziendelei...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is an intervention from hon. (Ms.) Saumu Sidi.

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you Mr. Speaker. I think the Member is saying very critical allegations here; he is saying and I quote “anatoa kitu kidogo na anatoa kitu kidogo”. Can he substantiate that?

Hon. Mbura: Nataka kuchukua fursa hii kusimama tena kusema ni madai ya wanakandarasi wakitulezea sisi waheshimiwa tukiwa tunadai kandarasi zetu zinachelewa kutekelezwa na wakidai hivyo mimi pia huwa nalihisi ingawaje siwezi nikataja ni nani. Hapo naomba msamaha. Lakini hayo ni maneno ambayo katika afisi ya Elimu ya *procurement* imetutatiza sana mpaka saa hii miradi mingi italala.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes Saumu (Sidi).

Hon. (Ms.) Sidi: I think he has not withdrawn; amesema ataomba msamaha.

Hon. Mbura: Nimeomba.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Proceed.

Hon. Mbura: Kwa hivyo mheshimiwa Spika ni vizuri hata mimi pia nikiwa kwa rekodi kwamba hali ile imenipata na ushahidi wa kutosha na karatasi niko nayo mpaka saa hii Mafisini haijapata mwanakandarasi.

Kwa hivyo hali zile ningepomba maelezo na mapendekezo ya kamati ziweze kufuatilizwa kwa haraka ili hii Idara ya Elimu iweze kurekebisha hali zile na miradi yetu itekelezwe kwa wakati unaostahili kabla ya mwezi wa sita. Asanteni.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you hon. Members. We now proceed to the Member for Mwanamwinga hon. Pascal Jacob Tuva.

Hon. Pascal: Thank you Mr. Speaker. I also take this opportunity to congratulate the committee for a very good Report because it has actually covered on many of the problems that have eaten into this department for a very long time. The findings and the recommendations are so good that when they are taken care of properly then we will be handling these problems. But again I feel like there is another finding that the committee did not consider; that the Education department is dependent on engineers from the roads department. So it is like these two Departments have an interactive role which should be taken care of properly so that work can be done in good time and accordingly.

You will find out that when a project is passed by the Education Department, drawings are done by the Roads Department. So when you go to the education department to enquire about a project, they put the blame on the roads side because they say engineers are the ones who are sleeping on their job. So as a House we need to sit down and come up with a way to handle this problem because it is like there is a blame game between the two departments.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

You will find out that when you go to the roads department they also give you reasons like they do not have enough workforce; it is like they are overburdened by the work that is there. So this is a problem that we need to sit down as a House and look for a solution. Again on the same, many allegations have come out from Members and we also need to investigate because the movement of documents in between departments is also wanting because you could see a document moving from one office to the other taking almost three or four months. Then you can imagine if it is not corruption then what is making these documents to...

(Hon. Ziro stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes hon. Peter Ziro, what is your Point of Order?

Hon. Ziro: Thank you Mr. Speaker. The Member on the floor is talking of documents being circulated in the Department of Education and according to the Report that has been tabled by the Chairperson; I think he has given us a very clear way forward and even the seconder and those who have debated. Can the Member substantiate which documents he is talking about and the delay if he knows anything that is going on in the Executive that we do not know as a House?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): So what is your Point of Order?

Hon. Ziro: I want him to clarify whatever he is saying Mr. Speaker.

Hon. Pascal: Let me respond to that. The documents I am talking about are the procurement documents because when a tender is floated, there are documents that move from one place to the other regarding the same tender. So if for example an LSO is not signed within the proper time, that is the document I am talking about and there are so many documents that are needed so that a project can move from the initial stage to the other. Therefore I think you are guided hon. Member. Those are the issues that we actually need to look into and solve.

The issue of corruption that has not been substantiated has cropped up from various Members and there is need for investigation to be done because the Members have interacted with the Executive and these are things that have floated in their minds as they interact with the other areas. So we also need to investigate that and come up with a proper way forward. I want to commend the committee for a job well done and we need to pin down the Executive to ensure that all that is within this Report is implemented for the betterment of Kilifi.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Hon. Member for Jaribuni

Hon. Maitha: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Nami nasimama kuunga mkono Ripoti hii. Kabla nitoe Hoja yangu naona ni vyema nisifu kamati haswa ikiwa inasimamiwa na mwenyekiti Mheshimiwa Daniel Chai Chiriba. Nilipitia hii Ripoti na kwangu mimi imegusa zile shida ambazo nilizipitia pale Jaribuni. Kwanza mwaka jana niliona niko na ECD 16 ambazo hazijakamilika moja wapo ikiwa ni ile iliyotajwa hapa ya Matolani. Mheshimiwa Spika ile ofisi ya elimu iko na njia nyingi fiche sababu ukifika pale ni kana kwamba hawana ufahamu wa kile kinaendelea lakini kwa ule muda mchache nimeandamana nao nimeona kuna njama fiche. Nikikupa mfano, Mheshimiwa Spika, kuna choo kilikuwa kinajengwa *Executive*; nilishangaa makaratasi yalipelekwa mbio mpaka mwana kandarasi akapatikana akapelekwa kwa *site* lakini hilo jambo la ECD mpaka ninavyoongea hapa karatasi yake hayajatoka. Sasa nilivyokuwa najaribu kuulizia kila mtu anataja mwenzake umesema tusitaje majina lakini huyu afisaa ametajwa hapa bado tuko na maswali naye kwa sababu utaenda atatajwa yeye atataja mwenzake sasa unaenda pale Mheshimiwa unazungushwa jambo ambalo si jema.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Sisi tunafikiri hawa ni wakaazi wa hapa kaunti ya Kilifi ni lazima wapende kaunti yao na waone wataisukuma vipi kwenda mbele. Mheshimiwa Spika ukiangalia miradi mingi ambayo inatengenezwa ama inajegwa ni ya hii sekta ya elimu; Kaunti ya Kilifi kama ni kusherehekea ugatuzi basi utapata miradi mingi kwa wananchi karibu kila mheshimiwa ambaye anasimamia wadi naona ni wachache lakini wengi lazima wawe na mradi wa ECD kwa kila bajeti yao. Kwa hivyo mwananchi kufaidi ugatuzi haswa kwa sekta ya elimu naona ni vyema miradi iwe itaweza kuendeshwa kwa wakati mzuri.

Tumekula mwaka wa 2018/2019 bajeti sasa tumefika awamu ya tatu ikiwa bado miradi haijaanza na bado mtashangaa kama watajenga wakati gani mpaka wamalize ndio sasa tukiwa tunapanga bajeti ya 2019/2020 kuona hiyo mirengo itafanyika vipi. Kuna mradi wa ECD kule Jaribuni unaitwa Mkomba-chemba ambao uliwekewa pesa mwaka wa 2015/2016 ukasukumwa mbele 2016/2017. 2018 ukapotea niliandika *Statement* hapa haikujibiwa lakini nataka kukwambia Mheshimiwa Spika juzi tukiwa kwa kamati yetu ya *Implementation* tuliandika barua kumuita Waziri ili kuja kuangalia haya maneno ya ECD na pia kueleza utendakazi wake kwenye ile ofisi ili tuone tutapiga hatuwa vipi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika tukienda na vyuo vya ufundi pia tunasema kwamba yale tunayoyajadili hapa mengi tumeona hayajatumizwa; tulikuwa tunaangalia hii Ripoti na tukaona walimu walikuwa waajiriwe tulishangaa tuko na maeneo bunge saba lakini waliajiri wanne na ukiangalia ile bajeti ilikuwa inaruhusu kuajiri wote saba kati ya wale wanne kila mmoja alipewa mbili au alipewa tatu. Bw. Matoka anasimamia eneo bunge la Ganze yeye ndio anasimamia Kilifi –South kwa hivyo tunajaribu kuona utendakazi wake haujakuwa mzuri na haujagusa pale chini. Tunaomba ikiwezekana Mwenyekiti, sisi tutakuja kumhoji Waziri lakini pia ulitilie mkazo ili tuone hawa watendakazi wa hivi vyuo vya ufundi wanaongezwa na tunapiga hatua. Asante Mheshimiwa Spika na naunga mkono Ripoti hii.

The Deputy speaker (Hon. Kenga): Thank you, the Vice Chairperson Culture.

Hon. Hadad: Thank you Mr. Speaker for giving me opportunity to make my submissions, but after going through the committee findings and the recommendations, I believe there is a serious issue going on the Executive part. First, I came across a lot of projects that were not completely done and secondly, they were not done at per the standard; they had cracks, etc. I do not know but I believe the Executive are supposed to be the supervisors of engineers and contractors. We have contracts which are done by the youth and if the County Government fails to pay their pharases in turn, how do you expect the youths to grow?

It will be in order to sermon those in charge of the payment and supervision of the contractors to this House so that they can directly answer to us because what they are doing is pathetic. This does not only happen to ECD's but this happens to a lot of constructions in this county. It is high time that we take it up and stop this from happening in the future. These people are letting us down because when you do inspection they are told to demolish the building and start afresh; when will our children go to study? When will we give equal opportunity to all if we are lagging behind with such stupid mistakes? Sorry for my vulgar language but I have to, it is really irritating to see such things in our findings. Is it possible that as early as next week we call these people to this House to answer to us?

(Hon. Pascal stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Pascal, what is your point of order?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Pascal: Mr. Speaker I think we are in a House of honour and we need to use what we call parliamentary language. So is the Member in order to actually point out on stupidity and whatever? I think he needs to kindly withdraw. Thank you.

Hon. Hadad: Am sorry but I believe stupidity is not an insult but a behavior so it is their behavior that is wrong and am not insulting them directly. Anyway let me proceed.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Hon. Member you are free to proceed. I mean he was referring to a mistake. The kind of mistake that he was referring to is stupid; he did not direct that one to an individual.

Hon. Hadad: Thank you Mr. Speaker. The procurement should know who to give the contracts to. It is their mistake for not checking the contractors perfectly in time. Mr. Speaker if I am in order I would like these officers to be called next week to give us direct answers to this, and I hope maybe it will be the end of everything.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. The Majority whip.

Hon. Mwayaa: Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi ambayo nimeomba kwa muda mrefu. Wacha nipongeze Kamati ya Elimu ya chekechea na vyo vya ufundi kwa kazi yao nzuri na ya kupendeza. Waliweza kutembelea vyo kidogo lakini kuna kwengine pia shule ziliisha zile *modern* kama kwangu na pia tuliweza kutembea sehemu za Marafa tukaona kuna shule nzuri sana ya kisasa; walifanya kazi nzuri ambayo ni ya kupendeza wacha niwape kongole.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili tuna kazi ya kufanya; kazi yetu ya uangalizi ama *oversight* itabidi ifanywe kwa bidii maanake kusema kweli kile kitengo cha uchoraji ama *works* na kile kitengo cha *procurement* itabidi tuwe kidogo na uangalifu wa makini. Wenzangu walitangulia wamesema kwamba wachoraji itabidi tuwaite waje watuelezee kuchora darasa moja inachukua muda gani; madarasa mawili inachukuwa muda gani kisha halafu procurement nao wawe wako pale. Mheshimiwa Spika, kuna kazi ambayo inakoseka ya madarasa ambayo yalichorwa kutoka mwaka wa 2013 hayajaisha. Ukifika kwa *procurement* wanakwambia kwamba ni *works* ambayo haijamaliza kuchora kwa hivyo kuna uwezekano Bunge hili la Kilifi liwaite hawa watu hasa *works* na hawa *procurement* tuwashikanishe watueleze kwa urefu ya kwamba kuchora darasa moja au mawili inachukuwa muda gani maanake kile ambacho kinafanyika Mheshimiwa Spika kama sijakosea *ni copy and paste*.

Kuna siku mimi nilipata stakabadhi zilizokuwa ni za shule ya sehemu nyengine inaitwa Kidzini North na wame *copy paste* na darasa lengine ambalo lilikuwa lijengwe sehemu ya Mwembeni. Kile kinachofanyika katika *department* ya *works* ni *copy and paste*; leo hii utapata kuwa *procurement* wanalaumu wale wengine na ukifika kule ni madarasa yale *standard*. Walisema darasa hili *standard* ni hii wana *copy and paste* na tungekuwa tunaenda mbio sana katika haya mambo ya ujenzi wa madarasa. Kwangu kuna madarasa mawili pale sehemu ya Katsangani simiti yaoza mifuko karibu ishirini; kisha wakasema kwamba wana *terminate* yule mwanakandarasi na mpaka saa hii hakujapatikana mwengine maanake wanasema ile *termination* kuna shida kidogo hali yaku *terminate*, kwa hivyo lazima twende kwa uharaka tuweze kuwaita hawa watu ili Kilifi iweze kufanya kazi.

Bunge hili lisitupe lawama kule; tuwaite hawa watu watuambie watafanya kazi kwa bidii ya aina gani ili kwamba tuweze kuhudumia watu wa Kilifi kwani vile tunaenda haipendezi, lakini nimesimama kuunga mkono; kazi ni nzuri na kama mliwaita, kama vile mnavyosema mliwaita nafikiri ipo haja ya kuwaita tena kama Kamati ya Nyumba Nzima ili waweze kuleta haya majibu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Jambo lengine Mheshimiwa Spika pale Kilifi unaambiwa kuna kitu kinaitwa *network* ambayo wanasema iko chini. Kilifi ni kubwa na kama *network* ya Kilifi pale *headquarter* ni haba wacha Mheshimiwa Spika tutafute *network* mahali iko tukapige kambi pale lakini tuhudumie watu wa Kilifi. Inaudhi Mheshimiwa Spika, mtu akijua kwamba hajafanya kazi yake anakwambia kwamba *network* ilikuwa iko chini haya yakiwa ni majibu tunapatiwa tuko tayari kama bunge hili tuseme ya kwamba tunapiga kambi; aidha tutaenda na matonabari mahali fulani ama mahema, tukapige kambi mahali ambako kuna *network*, na wajuzi wako wa kutafuta *network*. Kwa nini tuzuliwe na watu ambao kidogo wanataka kutudanganya? Naunga mkono kazi waliyofanya ni nzuri na sisi pia itabidi tufunge mikanda yetu vizuri ili pia tukabiliane na wale maafisaa ambao wamezembea katika kazi zao. Asante

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much the Majority Whip hon. Mwayaa and I want to believe the chairperson ICT was very attentive into the contributions because he was talking about the issues of network and the internet. I hope you have been able to get his contributions, but thank you very much it was on a light note. The Member for Mtepeni (Hon. Gogo) kindly proceed.

Hon. Gogo: Asante Mheshimiwa Spika ingawaje nimebonyeza kitambo mpaka yale niliyotaka kuzungumza waheshimiwa wenzangu wameyagusia sana. Pengine nisipoteze wakati kwanza nasema ya kwamba mimi naunga mkono mapendekezo ya kamati hii ambayo walipendekeza kwa kitengo hichi cha elimu. Mheshimiwa Spika, ombi langu nitaungana na Mheshimiwa Hadad ambaye amesema ya kwamba ni vyema kwa sababu ukiangalia *mood* ya *Members* wote wa Bunge ni kwamba sote hatukubaliani na utendaji kazi wa kitengo hiki cha elimu. Mimi ningeomba kama inawezekana kweli hawa wafanyikazi tuwaite Bungeni ili Bunge zima tuwe hapa na tuweze kuzungumza nao.

Mheshimiwa Spika ilikuwa imefikia mahali sisi kule nje ya Bunge tulikuwa tumekubaliana ya kwamba siku moja tuende asubuhi na mapema tukafunge ile ofisi ya elimu kwa sababu kule nje wananchi wanajua sisi viungozi waliotuchagua hawajui kuna watu wana *fail* kazi zetu kama waheshimiwa. Kwa hivyo naona kabla tufikie kiwango hicho kamati imependekeza tuchukue muda gani yawe yatafanyiwa kazi ili tuone mabadiliko? Kwa hayo machache naunga mkono hii Ripoti. Asante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Finally let us have contribution from Hon. (Ms.) Ngari

Hon. (Ms.) Ngari : Asante Mheshimiwa Spika kwa hii nafasi. Pia mimi naunga mkono Ripoti hii ya kamati na kusema kweli ile hali halisi iliyo mashinani upande wa elimu na kulingana na hii Ripoti kuhusu hayo majengo ya *ECD* ni mambo ya kusikitisha sana. Kama tutasimama tuseme elimu ni lazima na watoto wetu hawana mahali pa kusomea ina maana kwaamba hiyo elimu hata tukiilazimisha haitaenda vile ambavyo tunaihitaji. Kwa hivyo kuna haja kabisa na mimi naunga mkono maoni ya wale Waheshimiwa waliosema tuwaite hawa wahusika ili watupe majibu mwafaka ndio tupate ile miradi yetu kwa wakati unaofaa.

Ukiangalia hiyo Ripoti ni kama karibu kila *department* miradi ipo mpaka mwaka wa 2013/2014 ambayo haijatekelezwa sasa ina maana kwamba sisi tunapitisha hapa lakini kutekelezwa inakuwa shida. Kila mwaka tutakuwa tukirudia hilo jambo moja hatuendelei na wakaazi wa Kilifi watakuwa hawaoni manufaa ya Wabunge kuwa ndani ya Bunge na hawaoni maendeleo yakiendelea kule mashinani. Kwa hivyo tutakuwa ni kama tuko lakini hatufanyi ile kazi ambayo tunapaswa tuifanye. Kuna haja kabisa hawa wahusika waitwe na kujibu haya

maswali ndio hata Waheshimiwa wakiulizwa maswali kule mashinani tuwe tunaweza kujibu na wakaazi wa Kilifi wanaona maendeleo yakifanyika. Asanteni sana nimesimama kuunga mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon Mae.

Hon. Mae: Asante Mheshimiwa Spika. Kwanza niwape kongole wanakamati wakiongozwa na nduyu yangu pale kutoka kule Jilore mheshimiwa Daniel Chiriba. Mimi pengine niwapatie mfano wa eneo bunge letu la Rabai kabla ya mheshimiwa Mbunge wetu mheshimiwa Kamoti kuingia. Rabai ilikuwa kuna shida ya elimu kwa maana watu walikuwa kidogo; viwango vyao vya elimu viko chini. Mheshimiwa yule alipoingia akaanza kuboresha madarasa ya shule za msingi, hususan darasa la saba na la nane. Wao nao wakajipata wako katika mazingira yale yale unayoweza kuyapata katika zile shule kubwa kubwa. Nikisema hivyo ni kwamba darasa zuri lenye madirisha mazuri ya vioo, viyoyozi ndani na mahali pazuri pa kukalia. Mheshimiwa Spika baada ya mwaka mmoja, sisi tulikuwa tukizungumzia watoto kidogo wanaokwenda shule zile kubwa kubwa za upili; lakini baada ya miaka miwili ile namba ikaongezeka kwa sababu mtoto kila siku anatamani kwenda kukaa katika darasa lile zuri.

Ukija upande wetu wa Kaunti ni hali ya masikitiko kwa sababu, darasa hata usizungumzie mawili moja tu, linajengwa kwa takriban miaka mitano na pia lisiishe. Sisi tulivyokuwa katika kampeni tuliwaahidi wapiga kura wetu kwamba sisi tutakapoingia, huu uwezo ambao uko tukishinda wale wapinzani waliyokuwako tutabadilisha mambo kadhaa kwa sababu haiwezekani kwamba darasa lijengwe zaidi ya miaka mitano.

Mimi nikaona pengine ni yale madarasa ambayo yanapendekezwa na wale *Executive*. Nikasema wacha niweke pesa za wadi katika haya madarasa pengine tutajenga kwa haraka. Lakini kufikia sasa tunakaribia kufunga mwaka bado ugonjwa ni ule ule. Unapokwenda katika zile afisi husika unaambiwa *system* hazifanyi. Sasa sijui mimi ndio niingie katika mitandao ile nitengeze. Na hapa kaunti kuna mtu analipwa kuhakikisha ile mitandao masaa ishirini na nne inakuwa sawa.

Sasa tunaweza tukamlaumu ama tukalaumu maafisaa lakini pia tunapowalaumu tuangalie nani mhusika wa kuhakikisha hii mitandao yetu ya Kaunti inafanya kazi? Kwa sababu, wanasema kuna maagizo kutoka kwa Raisi kwamba kila mradi lazima upitie ile wanaita *e-procurement*. Sawa tumekubali lakini kule mashinani watoto wetu wanapata tabu; watoto wetu wanaumia na wengi wetu hapa walisoma zile nyakati za madarasa haba na wengine walisoma chini ya miti. Kwa hivyo unapokuwa na nafasi ya kubadilisha mazingira alafu pia nafasi ile ni kama kuna uzembe fulani watu wanaendeleza, inasikitisha na sisi kama Bunge isiwe tu ni stori tunaongea hapa ile kwamba Bunge limejadili halafu basi kila mtu afunge Ripoti aende zake.

Mheshimiwa Spika ningomba hatua zichukuliwe; tuwaite hawa wahusika na kama shida ni *contractor* watwambie. Sisi tunajua si ni ndugu zetu wengine lakini kama huna uwezo wa kusimamia mradi kwa nini upewe ati kwa sababu wewe ni ndugi yangu? Tupeane mtu ambaye atatuhakikishia atatujengea darasa ndani ya mwezi au miezi miwili aende adai pesa zake zote. Lakini hawa watu ajenge sijui mpaka wapi aende tena adai kitambo alipwe aje aendeleze, hawatatupeleka popote mheshimiwa Spika.

(There was power blackout in the Chamber)

(Hon. Mwarandu stood on a Point of Order)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a Point of Order from hon. Kombe Mwarandu.

Hon. Mwarandu: Thank you Mr. Speaker. It is not really a Point of Order on what the hon. Member is saying but I am worried. You remember on 15th January this year there was a terror attack in Nairobi and it is not normal for this House to have a black out for 3 of 10 minutes. I think somebody needs to enlighten us on what is happening in this House?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you for the concern that you are raising. The security of Members is very important and I hope there is action being taken to rectify the situation. Proceed.

Hon. Mae: Mheshimiwa Spika mimi naomba Bunge hili tuchukue hatua za haraka kama ni kumuita Waziri na msaidizi wake ili waje watueleze ile miradi yote ambayo haijakamilika itakamilika lini? Nikiwa mwanakamati wa Bajeti, sidhani kama wakitupa bajeti ama makadirio ya fedha ya kwamba tuwawekee kwa sababu ya kumaliza miradi ile sisi hatutakataa. Lakini waje watwambie wanahitaji muda gani ili waweze kumaliza ile miradi. Kwa hayo mengi mimi nasema asante na kongole kwa kamati ile.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much hon. Members for your candid contributions. The Chairperson Pre-primary Education and Vocational Training and the entire members of the Committee, I want to believe that you have been able to note the issues of grave concern as given out by Members and as you sit as a committee, you will be able to follow up on all the issues that have been raised and make sure that the projects are completed within the stipulated time. And for those projects that have already delayed then there must be a way to make sure that they are completed for better service delivery.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

There being no other business to transact, this House stands adjourned until afternoon at 2:30 p.m. Thank you.

The House rose at 11:10 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*